

# AZIMIO LA KUHIFADHI SIMBA

Sisi wote tunakubali kuwa simba wanaathiriwa na matatizo mengi na wako kwenye mzozo. Takriban asilimia hamsini ya idadi yao imeangamizwa katika kipindi cha miaka ishirini na tano iliyopita.

Hivi leo, ni simba elfu ishirini wamebakia kote barani Afrika.

Kwa hivyo, wajibu wetu mmoja ni kuhakikisha kuwa simba wa porini, maeneo wanamoishi na pia jamii za Afrika wanastawi kwa pamoja.

Tunatambua ya kwamba, marais na viongozi wa nchi za Afrika, pamoja na jamii zinazoishi karibu na makao ya simba ni walinzi halisi wa hao simba kwa niamba ya ulimwengu wote.

Vilevile, tunatambua ya kuwa Simba ni turadhi/hazina ya Kitaifa na Dunia. Tunafahamu basi, tukijitahidi tunaweza kuzidisha idadi ya simba wetu.

TUTAJIKAKAMUA:

## KUSITISHA KUANGAMIA KWA SIMBA

Lazima tuwalinde simba wetu, malisho yao ambao ni wanyama wengine wa pori sawa na makao yao.

## KUPUNGUZA GHARAMA

Lazima tuwapunguzie watu wa Afrika gharama nzito wanayobeba kwa kuishi karibu na simba.

## KUONGEZA DHAMANI

Lazima tujitahidi kueneza na kuongeza mafanikio tunayopata kutoka kwa simba, yenye faida za kitamaduni, kiuchumi na kimazingira barani Afrika, katika jamii zetu, uchumi wa kitaifa na kote duniani.

